HakiElimu
Muhtasari Na 1: 2011 K

# Nani huamua Watoto wetu Wajifunze Nini?

**Ripoti ya utafiti kuhusu uhusiano wa ubora wa mitaala na utoaji elimu bora**

*Huu ni muhtasari wa ripoti ya utafiti wa mahusiano kati ya ubora wa mitaala na utoaji elimu bora uliofanyika mwezi Agosti mwaka 2010. Utafiti huu ulifanyika katika wilaya sita za Tanzania bara. Ambazo ni: Monduli (Arusha), Mufindi (Iringa), Pangani (Tanga), Misungwi (Mwanza), Uyui (Tabora) na Bukombe (Shinyanga). Unashauriwa kusoma ripoti nzima ili kupata taarifa kwa kina.*

## 1.0 Utangulizi[1]

Katika dunia ya leo, ili binadamu aweze kuboresha maisha yake ni lazima awe na elimu. Elimu ndiyo inayomuwezesha kujitambua na kujimiliki yeye mwenyewe kwanza, kuzikabili changamoto zinazomsonga, kuyatawala na kuyatumia mazingira yanayomzunguka ili kuboresha maisha yake. Ndani ya utandawazi ***elimu kidogo tafsiri yake ni umaskini zaidi; na elimu zaidi tafsiri yake ni maisha bora zaidi.***

Nelson Mandela mwaka 1991 amewahi kusisitiza umuhimu wa elimu kwa maendeleo ya jamii, kwa kusema;

*"..elimu ni injini kubwa ya maendeleo ya mtu. Ni kupitia elimu ndipo binti wa mkulima mdogo anaweza kuwa daktari bingwa, kwamba mtoto wa kibarua wa mgodini anakuwa Mkuu wa Mgodi, na mtoto wa kibarua wa mashambani anakuwa Rais wa taifa kubwa".*

## 2.0 Malengo ya Utafiti

Katika kipindi cha miongo miwili iliyopita kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wazazi, serikali, sekta binafsi na asasi za kiraia juu ya 'kushuka' kwa ubora wa elimu nchini Tanzania. Kuna vigezo viwili vinavyotumika katika kupima kiwango cha ubora wa elimu.

Kwanza, wasomi hutazama ufaulu wa wanafunzi katika stadi za msingi kama vile kuandika, kusoma na kuhesabu (kujumlisha na kutoa). Pili, wasomi hutazama kiwango ambacho wanafunzi wameweza kupata stadi za msingi zitakazowawezesha kuukabili ulimwengu wa ajira. Nadharia hizi zinawaongoza wananchi wengi kuweka matarajio makubwa kwa watoto wao pindi wanapoandikishwa shule.

Lakini msingi mkuu wa utoaji elimu bora unajengwa na ubora wa mitaala pamoja na ubora wa mbinu, mikakati na jitihada za kutekeleza mtaala huo. Kwa kutilia maanani ukweli huu utafiti ulilenga mambo manne:-

**2.1** Kutathmini ubora wa mtaala wa elimu ya msingi na sekondari

**2.2** Kutathmini athari za kutumia kitabu cha aina moja au vingi

**2.3** Kutathimini ushiriki wa jamii katika kuhakiki ubora wa mtaala

**2.4** Kupata maoni ya wadau wa elimu kuhusu namna ya kuboresha mtaala ili kutoa elimu bora.

## 3.0 Mbinu za utafiti na sampuli ya maeneo

Mbinu za utafiti zilizotumika zinajumuisha mbinu mchanganyiko ambapo mbinu ya utafiti inayohusisha takwimu na ile isiyohusisha takwimu zilitumika katika ukusanyaji wa data. Maswali dodoso yalitumika ili kupata data zinazohusu tathmini ya walimu na wanafunzi katika utekelezaji wa mtaala katika shule zao. Vikundi vya majadiliano vilitumika ili kupata maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ubora wa mtaala pamoja na athari zake katika utoaji wa elimu bora. Vikundi vya majadiliano vilifanyika kwa wazazi pia ili kupata maoni na ushiriki wao katika maendeleo na utekelezaji wa mtaala. Mahojiano yalifanyika kwa watunga sera katika ngazi za mikoa na wilaya ili kupata maoni yao kuhusu ubora wa mtaala na jinsi gani unaathiri ubora wa elimu. Na pia vitabu vya kiada vilifanyiwa tathimini ili kubaini ubora wake.

Washiriki katika utafiti huu walitoka wilaya za Monduli (Arusha), Mufindi (Iringa), Pangani (Tanga), Misungwi (Mwanza), Uyui (Tabora) na

1 Kijarida hiki Kimeandaliwa na **Mtemi Gervas Zombwe**: HakiElimu. Ni ufupisho wa ripoti ya utafiti wa mahusiano kati ya ubora wa mitaala na utoaji elimu bora. Unashauriwa kusoma ripoti nzima.

Haki Elimu Utafiti-brief.indd 1 Saturday2April//2011 1:20 PM

Bukombe (Shinyanga). Katika kila wilaya, shule nne zilichaguliwa-mbili za msingi na mbili tena za sekondari. Shule zilichaguliwa kwa kuzingatia ufaulu katika Mitihani ya Kuhitimu Elimu ya Msingi na Mitihani ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari. Ufaulu wa juu zaidi, wa kati na ufaulu wa chini kabisa.

## 4.0 Mtaala ni nini na huathiri vipi elimu?


Waandishi wengi wanakiri juu ya ugumu uliopo katika kuelezea maana ya dhana mtaala. Neno mtaala linatokana na lugha ya Kilatini, likimaanisha 'kuendesha kozi'. Kwa kuzingatia maana ya asili ya neno lenyewe, Oliva (1997, uk 4) anaelezea maana ya mtaala kwa kuzingatia mambo 12. Mtaala kama:

- Kile kinachofundishwa shuleni
- Seti ya masomo
- Maarifa
- Programu ya masomo
- Seti ya vitu vya kujifunza
- Orodha ya kozi
- Seti ya malengo ya ufanyaji kitu
- Kozi ya kujifunza
- Kila kitu kinachoendelea shuleni, ukijumuisha mambo yanayofanyika nje ya darasa, usimamizi, na uhusiano kati ya mtu mmoja na mwingine
- Kila kitu kinachopangwa na wafanyakazi shuleni
- Mjumuiko wa uzoefu mbalimbali anaoupata mwanafunzi awapo shuleni
- Kile ambacho mwanafunzi hukipata kikiwa ni matokeo ya kuwa shuleni

## 5.0 Matokeo ya utafiti

### 5.1 Maoni ya walimu na wanafunzi juu ya ubora wa mitaala


**5.1.1 Uelewa wa walimu kuhusu sera muhimu za nchi.** Kwa hakika, mtaala wa elimu huongozwa na dira na mwelekeo wa nchi katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Na kwa maana hiyo ni muhimu kwa walimu kuelewa baadhi ya sera muhimu za nchi. Utafiti uligundua kuwa walimu wengi (75%) wanauelewa MKUKUTA na walimu wachache sana (34%) wanaelewa dira ya taifa ya maendeleo. (Tazama mchoro na 2).




*Mchoro 1: Asilimia ya walimu waliosema kwamba wanaelewa Dira ya Maendeleo Tanzania 2025 na MKUKUTA*


**5.1.2 Uelewa wa walimu kuhusu malengo ya elimu ya Tanzania.** Ni muhimu kwa walimu kuelewa malengo ya elimu kwa kuwa ndiyo msingi wa kutekeleza mtaala wa elimu. Kwa kuzingatia umuhimu huu, walimu waliulizwa ni kwa kiwango gani wanayaelewa malengo ya elimu ya taifa.

Idadi kubwa ya walimu (asilimia 86.8) waliripoti kwamba wanayaelewa malengo ya elimu vizuri zaidi, na walimu *(asilimia 13.2) wanayaelewa kiasi* malengo ya elimu ya Tanzania. (Tazama mchoro na 2).




*Mchoro 2: Asilimia ya walimu waliosema kwamba wao pamoja na wadau wengine wanayaelewa malengo ya elimu ya taifa*

**5.1.3 Maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufanisi wa mitaala ya elimu ya Tanzania.** Walimu na wanafunzi waliombwa kuonesha ni kwa kiwango gani mtaala wa elimu wa Tanzania unafaa katika kutoa wahitimu mahiri, wenye kujiamini, wanaowajibika na wenye ujuzi unaohitajika. Matokeo yanaonesha, idadi kubwa ya washiriki, walimu na wanafunzi, walisema kwamba mtaala wa elimu wa Tanzania hauna uwezo wa kutoa wahitimu mahiri katika nyanja mbalimbali. Kwa mfano, ni asilimia 35 tu ya walimu na asilimia 26 ya wanafunzi ndiyo walioripoti kwamba mtaala unafaa katika kuandaa wahitimu mahiri na wenye kujiamini. (Tazama mchoro 3).




*Mchoro 3: Asilimia ya walimu na wanafunzi waliosema kwamba mtaala unafaa katika kutoa wahitimu wanaojiamini, wanaowajibika, wenye tija na wenye ujuzi unaohitajika.*

## 5.2 Matokeo ya utafiti toka kwenye vikundi vya mjadala kuhusu ufanisi wa mitaala


**5.2.1 Mtaala wa sasa haukidhi matajwa ya jamii pana.** Wazazi walimu na wanafunzi walibainisha kwamba elimu iliyokuwa ikitolewa katika miaka ya 1980 na 1990 ilikuwa ikimwezesha mhitimu kuwa na mawazo ya kujitegemea katika ngazi yoyote ya elimu aliyofikia, na walibainisha pia kwamba elimu inayotolewa siku hizi inamfanya mhitimu ategemee zaidi 'kuajiriwa na kufanya kazi za ofisini'. Hii inatokana na mtaala wenyewe wa sasa ambao unatilia mkazo zaidi katika taaluma badala ya kutilia mkazo katika stadi za maisha. Kwa mfano, mmoja wao kati ya Maafisa wa Elimu wa Wilaya alisema:

*"...Kuna mkazo mkubwa katika kuhakikisha kwamba watoto wanafaulu mitihani na watoto wanafundishwa ili mradi tu wafaulu mitihani badala ya kuwafundisha jinsi ya kujitegemea. Hawaandaliwi kukabiliana na ulimwengu wa kazi."*

**5.2.2 Mabadiliko ya mara kwa mara ya mtaala yanavuruga utoaji elimu.** Walimu waliikosoa serikali kwa kuanzisha mtaala ambao hauendani na mahitaji ya watu. Pia waliukosoa mwenendo wa serikali katika miaka ya hivi karibuni ambapo imekuwa ikifanya mabadiliko ya mtaala bila ya kuwahusisha wadau ukijumuisha walimu na wanafunzi. Kwa mfano, Afisa Elimu wa Wilaya alikuwa na haya ya kusema kuhusu mabadiliko ya mtaala:


*"Nadhani tumekuwa tukifanya mabadiliko ya mtaala kiasi cha kuwachanganya walimu wetu. Kabla ya walimu hawajauzoea mtaala mpya, mabadiliko yanafanyika*

**5.2.3 Wanafunzi wanaridhika na jitihada za walimu wao.** Idadi kubwa ya wanafunzi walikuwa wakiridhishwa na uwezo wa walimu wao. Kwa mfano, asilimia 71 ya wanafunzi waliripoti kwamba walimu wao walikuwa na uwezo mzuri katika kuelezea dhana mbalimbali darasani (tazama mchoro 4).




*Mchoro 4: Asilimia ya wanafunzi walioripoti kwamba walikuwa wameridhishwa na uwezo wa walimu wao pamoja na upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia*

**5.2.4 Walimu na wanafunzi wanataka mfumo wa kitabu kimoja uendelee.** Katika utafiti huu, walimu walitoa mawazo yao iwapo wanapendelea matumizi ya vitabu vya aina moja vya kiada au vitabu vya aina nyingi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba asilimia 79.9 ya walimu wanapenda kutumia vitabu vya kiada vya aina moja katika shule zote, na asilimia 20.5 ya walimu wanapenda kuendelea na sera ya sasa ambapo vitabu vya kiada vya aina mbalimbali hutumika (tazama Mchoro 5).




*Mchoro 5: Maoni ya walimu kuhusu kutumia vitabu vya kiada vya aina moja au aina nyingi.*

**5.2.5 Walimu hawahusishwi katika kufanya mabadiliko ya mitaala.** Hii imewafanya wawe nyuma katika utekelezaji wa mitaala. Maana wao ndio watekelezaji wakuu wa mitaala.

## 5.3 Ushiriki wa jamii katika kufuatilia utekelezaji wa mitaala ni duni mno

**5.3.3** Wazazi wengi hawana uelewa kuhusu mitaala ya elimu ya Tanzania. Wazazi wengi waliohojiwa wanafahamu kidogo sana kuhusu mitaala na sera za

elimu za Tanzania. Na hii imewapa ugumu kufuatilia mchakato wa kujifunza na kufundisha.

**5.3.4 Wazazi hawashirikishiwi kwenye michakato ua utungaji mitaala.** Umuhimu wa ushiriki wa jamii katika maendeleo na utekelezaji wa mtaala hauwezi kupuuzwa. Ushahidi unaonesha kwamba kadri familia na jamii inavyoshirikishwa zaidi ndipo mafanikio ya wanafunzi yanavyopatikana zaidi (Niemiec, Sikorskim na Walberg, 1999). Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba wazazi na jamii kwa ujumla wanahusishwa kwa kiwango kidogo sana kwenye michakato ya utungaji wa mtaala. Na hii inaathiri elimu nchini.

### 5.4 Vitabu vingi vya Kiada vinavyotumika shuleni vina makosa

**5.4.3** Baadhi haviendani na mihtasari rasmi ya wizara, mada zimeandikwa bila kufuata maelekezo ya mtaala. Na hivyo vimekuwa vikipotosha wanafunzi

**5.4.4** Baadhi ya vitabu vina makosa makubwa ya kimaudhui. Na hivyo kuwafanya wanafunzi washindwe kuunganisha kinachofundishwa na kile wanachotarajia kupata.

**5.4.5** Baadhi ya vitabu vina makosa mengi ya lugha. Hivyo, mwanafunzi kushindwa kuelewa nini kinazungumziwa kwa manufaa yapi

## 6.0 Hitimisho/Mapendekezo

Upatikanaji wa elimu bora unategemea uwepo wa nyenzo bora za kufundishia na kujifunzia pamoja na ushiriki wa wadau muhimu katika michakato ya maendeleo na utekelezaji wa mtaala. Ili kuboresha michakato ya maendeleo na utekelezaji wa mtaala, mapendekezo yafuatayo yametolewa na wadau wa elimu:

**6.1** Mfumo wa matumizi ya vitabu vya aina nyingi hauna tija kwa kuwa unawafanya wanafunzi wajifunze dhana zinazotofautiana wakati wakitarajiwa wafanye mtihani wa aina moja. Hivyo, wananchi wengi, wazazi, walimu na wanafunzi walipendekeza matumizi ya vitabu vya aina moja na kwa hiyo serikali inapaswa kuliangalia hili kwa faida ya wote.

**6.2** Kuna haja ya kudhibiti ubora wa vitabu ili kuhakikisha kuwa vitabu vinavyopendekezwa kutumika mashuleni vinakuwa na ubora unaohitajika.

**6.3** Ukosefu wa nyenzo na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ulionekana kama kikwazo katika utekelezaji wa mtaala. Kuna haja kwa wasimamizi katika sekta ya elimu kutilia mkazo suala la upatikanaji wa nyenzo za kutosha za kufundishia na kujifunzia katika shule zetu.

**6.4** Hatua madhubuti zichukuliwe na wadau wa elimu ili kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa watoto ili wajifunze na wafanikiwe kitaaluma na kijamii.

**6.5** Walimu wafahamishwe kuhusu sera hizi pamoja na kupewa mafunzo ya mara kwa mara ili kupanua uelewa wao.

**6.6** Kuna haja ya kuboresha mbinu za ufundishaji ili zilenge kuwafanya wanafunzi wapate ujuzi unaohitajika katika mazingira ya sasa. **Suala la elimu ya kujitegemea ni hitaji la wananchi wengi**.

**6.7** Kuboresha maslahi ya walimu pamoja na kuwapatia mafunzo ni jambo muhimu katika upatikanaji wa elimu bora.

**6.8** Kwa kuwa Kamati ya Uidhinishaji wa Vitabu vya Kiada (EMAC) ndiyo chombo kikuu katika kuhakikisha ubora wa vitabu katika shule zetu, kamati hiyo inapaswa ifanyiwe maboresho. Hii ni kwa sababu vitabu vingi vya kiada ambavyo vimepitishwa na kamati hiyo vina makosa ambayo yanawapotosha walimu na wanafunzi.

**Tukitekeleza kwa vitendo, kwa pamoja na kwa dhamira safi tunaweza kuboresha elimu na maisha ya watanzania.**

HakiElimu inawezesha wananchi kuleta mabadaliko katika elimu na demokrasia.

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org

Haki Elimu Utafiti-brief.indd 4 Saturday2April//2011 1:20 PM